Taarifa Mpya Muhimu & Taarifa Kuhusu Mafunzo ya Kuhudhuria Kibinafsi

Huku kundi yetu ya kwanza ya wanafunzi ikipangiwa kurejelea kwa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi Jumatatu, Februari 22, na kundi letu la pili likirejelea mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi Machi tarehe 1, hii ndiyo taarifa muhimu na makumbusho ya kusaidia kuongoza mafamilia katika mpito:

Ni Kina Nani Wanarejelea Mafunzo ya Kuhudhuria Kibinafsi?
• **Februari 22 -** Wanafunzi katika in programu za elimu maalum zilizo tofauti zaidi na masomo ya kawaida ambao hapo awali walikuwa wanashiriki katika muundo wetu wa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi (wale wanafunzi ambao bado walikuwa wanashiriki katika mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi katika mwezi wa Disemba)

• **Machi 1 -** Wanafunzi, ambao hawako katika programu za elimu maalum zilizo tofauti zaidi na masomo ya kawaida, lakini ambao hapo awali walihudumiwa katika muundo wa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi majira haya ya mapukutiko kama mpango wetu wa awali wa kufungua shule upya.

• **Aprili 1** - Tarehe tunayolenga kupanua mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi kwa wanafunzi zaidi ya wale waliopangiwa kwa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi mwanzo wa mwaka huu wa shule. Tutaendelea kukuarifu kwa undani na kuhusu uwezekano wa kutimiza lengo letu la tarehe ijayo.

Usafirishaji
Kwa wanafunzi wanaorejelea mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi mnamo Februari 22 na Machi 1 wanaopokea usafirishaji, jadwali ya usafirishaji itaendelea kuwa sawa na wakati wa mwisho waliokuwa wakihudhuria shule katika muundi wa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi majira haya ya mapukutiko hapo awali.

Jopo la LPS la Muhtasari wa COVID-19
Taarifa ya mwisho kabisa ya COVID-19, taarifa mpya na taarifa zinginezo zinaweza kupatikana katika Jopo la LPS la Muhtasari wa COVID-19. Tafadhali angalia rasilimali hii muhimu ya taarifa.

Programu ya Kupima COVID-19
Kama sehemu ya mchakato ya kufungua upya, tutakuwa tukifanya kipimo cha kila wiki cha COVID-19 cha bure. Kipimo hiki kitapunguza hatari ya kuambukiza COVID-19 kwa kusaidia kutambua matukio yaliyo na maradhi katika watu ambao hawadhihirishi dalili zozote za COVID-19. Ili kushiriki, wazazi/walezi watatakiwa kutia saini fomu ya idhini kwa mtoto wao. Bonyeza hapa kwa fomu ya idhini.

Kipimo hiki cha COVID-19 ni ya upesi, rahisi na isiyo na maumivu. Ni kipimo cha pua ambacho hufuta ndani ya tundu la pua. Tutaweza kuwarahisishia zaidi mahitaji yote ya wanafunzi ili waweze kuwa na starehe katika kipimo.

Kipimo ni cha bure. Hufai kulipia au kuwa na bima ili kupimwa.
Idadi ya wanafunzi na wafanyikazi wanaoshiriki ikizidi, usalama katika shule zetu utazidi. Tafadhali bonyeza hapa ili kusoma zaidi kuhusu program hii ya kupimwa.

Chanjo ya COVID-19
Massachusetts kwa sasa iko katika Awamu ya 2 ya ufunuzi wake wa COVID-19. Kufikia muda wa chapisho hili, makundi yafuatayo yanatahiki kupata chanjo ya COVID-19: kila mtu katika Awamu ya 1; watu walio na umri wa 75 au zaidi; wanafunzi walio na umri wa 65 na zaidi; wakaazi na wafanyikazi wa nyumba za ulezi wa wazee ya bei nafuu; watu walio na zaidi ya magonjwa 2. Wale wanaoongoza wakaazi walio na umri wa 75 na zaidi ili kupokea chanjo pia wanaweza kupokea chanjo. Wafanyikazi wa masomo ya utoto na chekechea hadi 12 sasa wanapangiwa kutahiki chanjo baadaye katika Awamu ya 2. Kwa taarifa zaidi kuhusu chanjo ya COVID-19, tembelea tovuti la jimbo.

Pia, angalia rasilimali hizi muhimu za taarifa kutoka Lowell Community Health Center (Kituo cha Afya ya Jamii ya Lowell) na Greater Lowell Health Alliance (Muungano wa Afya wa Sehemu kubwa ya Lowell):

- Jua ni Mambo Gani ya Ukweli na ya Uwongo Kuhusu Chanjo za COVID-19
- Sasa tuna chanjo mbili za kutulinda kutokana na COVID-19 - Haya ndiyo unayofaa kujua

Itifaki za Barakoa ya Uso na Miongozo ya LPS
Wanafunzi, wafanyikazi, na watu wowote wanaoingia shuleni mwetu wanahitajika kuvaa kifunika uso, ila iwapo kuna barua la thibitisho la kutovaa. Barakoa huweza kupunguza kasi ya usambazaji wa virui na huweza kulinda dhidi ya usambazaji wa virusi kutoka mtu aliye na virusi na asiye na dalili. Tafadhali rejelea Itifaki za Barakoa ya Uso na Miongozo ya LPS.

Itifaki za Usafishaji wa COVID-19
Huku wanafunzi wakirejea shuleni, tutaweza kuhakikisha tunafuata miongozo mikali ya usalama ili kuweza kulinda usalama wa wanafunzi na wafanyikazi wetu. Mitambo za kunadhifisha hewa zitaangaliwa kuhakikisha kwamba zinafanya kazi inavyofaa, vituo vya kemikali za kusafisha mikono na visafisha mikono vya darasa vitajazwa, na madawati na kila sehemu za shule zitasafishwa kila mara.

Wafanyikazi wetu wengine wataendelea kuchukua hatua za usafishaji kuondoa virusi katika mijengo yetu, kwa mfano kutumia mitambo ya kunyunyiza kemikali ya kuua virusi, haswa wakati mtu aliye na maradhi ya COVID ametambuliwa.

Unachofaa Kufanya Unaposikia Vibaya
Je unasikia vibaya au una dalili za COVID-19? Tafadhali rejelea cheti hiki cha usaidizi kilicho rahisi kufuata kwa miongozo kuhusu iwapo unafaa kuenda shule na muda unaofaa kujitenga au kuingia karantini iwapo una madalili au ulikuwa karibu na mtu aliye na COVID-19. Tafadhali hakikisha umewasiliana na muuguzi wa shule yako iwapo mtoto wako atadhihirisha dalili za COVID au kama alitambuliwa kama mtu aliyekuwa karibu na mgonjwa au kama alipatikana na kipimo kuwa na COVID.

Amri ya Kusafiri ya Massachusetts ya COVID-19
Tafadhali kuwa na ufahamu kuhusu Amri ya Kusafiri ya COVID-19 ya jimbo iwapo ulisafiri nje ya jimbo katika wiki ya likizo ya Februari, haswa kwa familia ya wanafunzi wanaorejea Februari 22 au Machi 1. Upungufu unaoendelea wa maradhi ya COVID-19 ni muhimu ili kuweza kuendelea kuwasomesha wanafunzi wetu shuleni.